# KIDATO CHA PILI
# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

**1 Ufahamu**.

(a) Alisingiziwa kumuua mtu.

(b) - Wafungwa hudhulumiwa

- Kuna uvundo
- Hakuna hewa safi
- Watu hawaogi
- Kuna giza na joto
- ( Kuna rundo la wafungwa (msongamano) *(zozote 1 x 4 = al 4)*

(c) Wasomi ambao wamepewa majukumu ya kuwakilisha maslahi ya raia ndio wanaowadhulumu. *(1 x 2 = al 2)*

(d) Hakuamini alikuwa kweli kaachiliwa huru.
Alihofia kuamuriwa asimame.
Alihofia kushukiwa bunduki. *(1 x 3 = al 3)*

(e) (i) Mwema
(ii) Mwadilifu
(iii) Mkweli *Zozote mbili (1 x 2 = al 2)*

(f) (i) Kitu kilichowazi. *(1 x 1 = al 1)*
*(ii)* Hamu kubwa ya kufurahia kitu. *(1 x 1 = al 1)*

**SARUFI**

a) /y/-kiyeyusho,hutamkiwa kwenye kaakaa gumu; /z/ -kikwamizo, hutamkiwa ufizini /t/-kipasuo, hutamkiwa ufizini; /h/-kikwamizo, hutamkiwa kwenye koromeo (1x4=4)
b) Madovu yamezaa madama makubwa sana. 1x2=2
c) M-ti/m-kebe/m-ke 1x1=1
d) Tupa (kifaa cha kunolea kisu) na "air conditioner" huuzwa bei ghali.2x1=2
e) Waandike insha ndefu! 1x2=2
f) Mjomba aliniambia kuwa ingenibidi kurauka alfajiri iwapo nilitaka kusafiri naye siku ambayo ingefuata. 1x2=2
g) Chebet alitoka garini na kufungua kioo. 2x1=2
h) Sentensi-neno-silabi-sauti 4x0.5=2
i) A-nafsi ya tatu umoja
-li-wakati uliopita
-nyw-mzizi
-ew-kauli ya kutendewa
-a. -kiishio
} mofimu tegemezi
Maziwa-mofimu huru kuainisha alama 1, kutaja alama 2=3
j) -ta- wakati ujao
-me- hali timilifu



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – NairobTel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

-li- wakati uliopita 1x3=3

k) mtahini/mtihani/mtahiniwa/utahini 2x1=2

l) A-WA 1x1=1

m) kilinge cha wachawi kilitiwa mbaroni jana 1x1=1

n) Watoto wao walilelewa kwenye koo hizi. 1x2=2

o) wakulima wakipalilia mahindi yao watapata mazao mengi.

p) S-KN +KT
KN-N
N-Mwanahamisi
KT-T+N+V+E+E
T-alilishona
N-rinda
V-lake
E-vizuri kila kijisehemu nusu alama=4

q) wa-nafsi ya tatu wingi
-li-wakati uliopita
-o- kirejeshi
-chez-mzizi
-ew-kauli
-a. kila kijisehemu nusu alama=3s

**ISIMUJAMII**

a) Dini-maandiko yanasema…. 1x2=2
b) -lugha ya heshima
-lugha ya upole
-matumizi ya msamiati maalum mf Amen, Halleluyah
-lugha shawishi
-huchanganya ndimi
-hunukuu na kurejelea vitabu vitakatifu km biblia, qurani
-lugha yenye vitisho
-aghalabu huwa na ukalimani 4x2=8
Tanbihi : Mwalimu akadirie mifano

**FASIHI SIMULIZI**

Sifa za hadithi
-huwa na wahusika mbalimbali k.v. binadamu, Wanyama, mazimwi, miti nk
-huelezea matukio kwa mpangilio wa moja kwa moja, kuanzia tukio la kwanza hadi la mwisho
-hutumia lugha ya kimaelezo/nathari
-huwa na mtendaji/fanani.fanani anaweza kuiga wahusika katika hadithi anayoisimulia
-hadithi husimulia matukio ya kweli au ya kubuni yenye maadili mf hekaya, za mazimwi na visasili ni za kubuni huku mighani na visakale vina ukweli Fulani



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – NairobTel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

-huwasilishwa kwa hadhira hai
-huwa na pahali maalum pa kutambia.
-baadhi huwa na fomyula maalum za ufunguzi na za kumalizia.
Zozote 5x2=10

Sifa za mtambaji bora
-huwa na ubunifu wa kiwango cha juu ili aibuni hadithi upya kila anapoitamba
-anapaswa kuijua hadhira yake na mahitaji yake yote
-anaelewa na kuimudu lugha ya hadhira yake
-anapaswa kuyaelewa mazingira ya hadhira yake na kutoa mifano inayofahamika
-anapaswa kujua utamaduni wa hadhira yake ili asiyavuruge mawasiliano
-anapaswa kuwa na uwezo wa ufaraguzi.
-anapaswa kuwa mcheshi
-anapaswa kuwa na uwezo wa kushirikisha hadhira yake
-Anapaswa kuwa mbaraza anayeingiliana vyema na watu/mhalaka mwema



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – NairobTel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**Hii ni insha ya maelezo**

Mwanafunzi ajikite katika kuhifadhi mazingira

Akishughulikia jambo linguine amepotoka kimaudhui

Baadhi ya hoja zinazotarajiwa:

- Kupanda miti kusiko na miti na kule kulikofyekwa misitu
- Elimu itolewe kuhusu madhara ya kuharibu mazingira
- Kukagua viwanda na hatua za kisheria kuchukuliwa kwa wanaokiuka utunzaji wa mazingira
- Askari kulinda misitu
- Kutumia kawi mbadala na zisizochafua mazingira
- Kufuga mifugo kulingana na eneo la malisho
- Kutolima kando ya mito
- Utumizi wa magari ya umma
- Kutumia taka kama malighafi tena

**MWONGOZO WA KUDUMU**

**UTANGULIZI.**

Karatasi hii imedhamiria kutathmini uwezo wa mtahiniwa wa kuwasiliana na msomaji na kuwasilisha ujumbe kimaandishi,akizingatia mada aliyopewa. Mawasiliano haya yatategemea ukwasi wa lugha ya mtahiniwa, kwa mfano, kutunga sentensi sahihi zenye mtiririko mzuri kimawazo, lugha ya kuvutia na yenye mawazo asilia, ubunifu mwingi na hati nadhifu. Kwa kutegemea maagizo ya swali lenyewe na umahiri wa lugha, ni lazima kutilia mkazo mtindo, mada na uwezo wa mtahiniwa kufuata maagizo vilivyo. Mtahini lazima aisome insha yote huku akizingatia sarufi, hijai, hoja, msamiati na mtindo ili aweze kuikadiria kwa kurejelea viwango mbalimbali vilivyopendekezwa. Viwango vyenyewe ni A, B, C na D kutegemea uwezo wa mtahiniwa.

**VIWANGO MBALIMBALI.**

**KIWANGO CHA D KWA JUMLA MAKI 01-05.**

i) Insha haieleweki kwa vyovyote vile ama uwezo wa mtahiniwa wa kutumia lugha ni hafifu sana, hivi kwamba mtahinilazima afikirie kile mtahiniwa anachojaribu kuwasilisha.
ii) Mtahiniwa hana uwezo wa kutumia maneno ya Kiswahili kwa njia inayofaa.
iii) Lugha imevurugika, uakifishaji haufai na insha ina makosa ya kila aina.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – NairobTel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

iv) Kujitungia swali na kulijibu.
v) Insha ya urefu wa robo ikadiriwe hapa.
**NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA D**.
D- (D YA CHINI) MAKI 01-02.
i) Insha haina mpangilio maalum na haieleweki kwa vyovyote vile.
ii) Kujitungia swali tofauti na kulijibu.
iii) Kuandika kwa lugha isiyo Kiswahili au kuchanganya ndimi.
iv) Kunakili swali au maswali na kuyakariri.
v) Kunakili swali au kichwa tu.
D WASTANI MAKI 03.
i) Mtiririko wa mawazo haupo.
ii) Mtahiniwa amepotoka kimaudhui.
iii) Matumizi ya lugha ni hafifu mno.
iv) Kuna makosa mengi ya kila aina.
D+ (D YA JUU) MAKI 04-05.
i) Insha ya aina hii hukuwa na makosa mengi ya kila aina, lakini unaweza kutambua kile ambacho mtahiniwa anajaribu kuwasilisha.
ii) Hoja hazikuelezwa kikamilifu/ mada haikukuzwa vilivyo.
iii) Mtahiniwa hana uhakika wa matumizi ya lugha.
iv) Mtahiniwa hujirudiarudia.
v) Insha itakayozingatia sura lakini ikose maudhui ikadiriwe hapa.
**KIWANGO CHA C KWA JUMLA MAKI 06-10**.
i) Mtahiniwa anajaribu kuishughulikia mada japo hakuikuza na kuiendeleza vilivyo.
ii) Mtahiniwa anawasilisha ujumbe kwa njia isiyovutia
iii) Mtahiniwa anaakifisha sentensi vibaya.
iv) Mtiririko wa mawazo unaanza kujitokeza japo kwa njia hafifu.
v) Insha ina makosa mengi ya sarufi, ya msamiati na ya tahajia (hijai).
C- (C YA CHINI) MAKI 06-07.
i) Mtahiniwa ana shida ya kuwasilisha na kutiririsha mawazo yake.
ii) Mtahiniwa hana msamiati wa kutosha wala miundo ya sentensi ifaayo.
iii) Mtahiniwa anafanya makosa mengi ya sarufi, ya hijai na ya msamiati na insha yake haieleweki kwa urahisi.
C WASTANI MAKI 08.
i. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe lakini kwa njia hafifu.
i) Dhana tofauti tofauti hazijitokezi wazi.
ii) Mtahiniwa hana ubunifu wa kutosha.
iii) Mtiririko wa mawazo ni hafifu na hana ufundi wa lugha unaofaa.
iv) Anajaribu kushughulikia mada aliyopewa.
v) Mtahiniwa ana shida ya uakifishaji.
vi) Mtahiniwa anafanya makosa mengi ya sarufi, ya hijai na ya msamiati lakini bado insha inaeleweka.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – NairobTel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

C+ (C YA JUU) MAKI 09-10.
i) Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri akizingatia mada lakini kwa njia isiyo na mvuto.
ii) Dhana tofauti tofauti zimejitokeza japo kwa njia hafifu.
iii) Kuna mtiririko wa mawazo japo hana ufundi wa lugha unaofaa.
iv) Misemo na methali zimetumika kwa njia hafifu.
v) Ana shida ya uakifishaji.
vi) Kuna makosa ya sarufi, ya msamiati na ya hijai yanayoathiri mtiririko wa mawazo.
**KIWANGO CHA B KWA JUMLA MAKI 11-15**
i) Mtahiniwa anaonyesha hali ya kuimudu lugha.
ii) Mtahiniwa anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi vizuri.
iii) Mtahiniwa ana uwezo wa kutumia lugha kwa ufasaha.
iv) Mada imekuzwa na kuendelezwa kikamilifu.
v) Insha ya urefu wa robo tatu ikadiriwe katika kiwango hiki.
**Ngazi mbalimbali za kiwango cha B.**
B- (B YA CHINI) MAKI 11-12
i) Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri kwa kueleza hoja tofauti tofauti akizingatia mada.
ii) Mtahiniwa ana mtiririko mzuri wa mawazo.
iii) Mtahiniwa anatumia mifano michache ya msamiati unaovutia.
iv) Makosa yanadhihirika kiasi.
B WASTANI MAKI 13
i) Mtahiniwa anadhihirisha hali ya kuimudu lugha.
ii) Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika akizingatia mada.
iii) Mtahiniwa anateua na kutumia mifano michache ya msamiati mwafaka.
iv) Sarufi yake ni nzuri.
v) Makosa ni machache/ kuna makosa machache.
B+ (B YA JUU) MAKI 14-15
i) Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika na anajieleza waziwazi.
ii) Mtahiniwa anawasilisha ujumbe kwa njia inayovutia na kwa urahisi akizingatia mada.
iii) Mtahiniwa ana mchanganyiko mzuri wa msamiati unaovutia.
iv) Sarufi yake ni nzuri.
v) Uakifishaji wa sentensi zake ni mzuri.
vi) Makosa ni machache ya hapa na pale.
**KIWANGO CHA A KWA JUMLA MAKI 16-20**
i) Mtahiniwa ana ubunifu wa mawazo yanayodhihirika na kutiririka akizingatia mada.
ii) Mtahiniwa anadhihirisha ujuzi wa lugha yenye mnato.
iii) Ana uwezo wa kutumia tamathali za usemi ili kutoa hisia zake kwa njia bora na kwa urahisi.
iv) Umbuji wake unadhihirisha ukomavu na ukakamavu wake kimawazo.
v) Insha ina urefu kamili.
**USAHIHISHAJI NA UTUNZAJI KWA JUMLA**.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – NairobTel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

Mtahini ni sharti aisome insha yote akizingatia vipengee muhimu. Vipengee hivi ni maudhui, msamiati, mtindo, sarufi na hijai.

**MAUDHUI**.

Maudhui ni hoja au mambo yanayozungumziwa, kuelezewa au kuhadithiwa kwa mujibu wa mada iliyoteuliwa. Maudhui ndio hasa uti wa mgongo wa insha yoyote ile. Ubunifu wa mtahiniwa hukisiwa kwa kutathmini uzito wa maudhui yake kulingana na mada teule.

**MSAMIATI**.

Msamiati ni jumla ya maneno yatumiwayo katika lugha husika. Mtahiniwa anatarajiwa kutumia msamiati unaooana na mada teule. Kutegea ukwasi wa lugha alionao, mtahiniwa anatarajiwa kuikuza mada kwa kuifinyanga lugha kiufundi. Ni muhimu kuelewa kwamba kutokana na maendeleo na ukuaji wa teknolojia na mawasiliano, maneno mapya yanaibuka kila uchao.

**MTINDO**.

Mtindo unahusu mambo yafuatayo:

- Mpangilio wa kazi kiaya.
- Mtiririko na mshikamano wa mawazo kiaya na katika insha nzima.
- Hati nzuri na inayosomeka kwa urahisi.
- Matumizi ya tamathali za usemi, kwa mfano methali, misemo, jazanda na kadhalika.
- Kuandika herufi vizuri kwa mfano Jj, Pp, Uu, Ww na kadhalika.
- Sura ya insha.
- Unadhifu wa kazi ya mtahiniwa.

**SARUFI**.

Sarufi ndio msingi wa lugha. Ufanisi wa mawasiliano hutegemea uwezo wa mtahiniwa wa kutunga sentensi sahihi zenye uwiano wa kisarufi. Mtahini ataonyesha makosa yote ya sarufi yaliyo katika insha anayosahihisha. Makosa ya sarufi huweza kutokea katika:

Matumizi ya alama za uakifishaji.

1. Kutumia herufi kubwa na ndogo mahali pasipofaa.
2. Matumizi yasiyofaa ya ngeli na viambishi, viunganishi, nyakati, hali, vihusiano na kadhalika.
3. Mpangilio wa maneno katika sentensi.
4. Mnyambuliko wa vitenzi na majina.
5. Kuacha neno linalohitajika au kuongeza neno lisilohitajika katika sentensi.
6. Matumizi ya herufi kubwa katika:

a. Mwanzo wa sentensi.

b. Majina ya pekee.

i. Majina ya mahali, miji, nchi, mataifa na kadhalika.

ii. Siku za juma, miezi n.k

iii. Mashirika, masomo,vitabu n.k

iv. Jina la mungu.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – NairobTel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

v. Majina ya kutambulisha hasa wanyama wa kufugwa, kwa mfano yale ya mbwa- Foksi, Jak, Popi, Simba,
Tomi na mengineyo.

**MAKOSA YA HIJAI/TAHAJIA**.

Haya ni makosa ya maendelezo. Mtahini anashauriwa asahihishe huku akiyaonyesha yanapotokea kwa mara ya kwanza tu.

Makosa ya tahajia huweza kutokea katika:

Kutenganisha neno kwa mfano ‗aliye kuwa‘
Kuunganisha maneno kwa mfano ‗kwasababu‘
Kukata silabi visivyo afikapo pambizoni kama vile ‗ngan - o‘.
Kuandika herufi isiyofaa kwa mfano ‗ongesa‘ badala ya ‗ongeza‘
Kuacha herufi katika neno kwa mfano ‗aliekuja‘ badala ya ‗aliyekuja‘
Kuongeza herufi isiyohitajika kama vile ‗piya‘ badala ya ‗pia‘
Kuacha alama inayotarajiwa katika herufi kama vile j i
Kukosa kuandika kistari cha kuendelezea neno afikiapo pambizoni au kukosa kukiandikia mahali pasipofaa.
Kuacha ritifaa au kuiandikia mahali pasipofaa, kwa mfano ngombe, ngom‘be, n‘gombe, ngo‘mbe n.k
Kuandika maneno kwa kifupi kama vile k.v, k.m, v.v, n.k na kadhalika.
Kuandika tarakimu kwa mfano 27-08-2010.

**UKADIRIAJI WA UREFU WA INSHA.**

Maneno 9 katika kila mstari – ukurasa moja na nusu.
Maneno 8 katika kila mstari – ukurasa moja na robo tatu.
Maneno 7 katika kila mstari – kurasa mbili.
Maneno 6 katika kila mstari – kurasa mbili na nusu.
Maneno 5 katika kila mstari – ukurasa mbili na robo tatu.
Maneno 4 katika kila mstari – kurasa tatu na robo tatu.
Maneno 3 katika kila mstari – kurasa nne na nusu.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – NairobTel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com